JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI KILINDI ASILIA

S.L.P 49

SONGE-KILINDI

SIMU NO: 0757 594915

JINA LA MWANAFUNZI :..........................................................

**YAH: MAAGIZO MUHIMU YAKUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KILINDI ASILIA MWAKA 2021**

Ninayofuraha kubwa kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2021 katika shule hii. Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kufika shuleni tareahe iliyopangwa bila kuchelewa. Shule imesajiliwa na wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi. Namba ya usajili ni S.4006. Kituo cha mtihani ni S.4697.

## MAHALI SHULE ILIPO.

Shule ya sekondari kilindi Asilia ipo katika makao makuu ya kata ya KILINDI katika Kijiji cha kilindi jirani na soko la kilindi,umbali wa km 23 kutoka kwinji na km 1 kutoka kilindi hadi shule ilipo.

## MAONO YA SHULE

Kuifanya Shule ya Sekondari Kilindi Asilia kuwa kituo cha kutolea Elimu

## WITO WA SHULE

Nidhamu, KazinaElimudaima (Displine,Work and Education forever)

**MICHEPUO**

Shule niya michepuo wa sayansi na Sanaa

Masomoyanayofundishwani:-

I. mathematics
II. Chemistry
III. Physics
IV. Biology
V. English
VI. Civics
VII. Kiswahili
VIII. History
IX. Geography

**SARE ZA SHULE**

- **WAVULANA**
  I. Shati mbili zenye mikono mifupi
  II. Suruali mbili zenye RINDA mbili RANGI ya kijana
  III. Tai mbili ziwe rangi ya suruali (TAI NDEFU)
  IV. Mkanda wa suruali mweusi wenye chuma ndogo
  V. Viatu vya Ngozi vyenye rangi nyeusi vyakufunga kwa gidamu visiwe safari boot wala vyenye visigino virefu
  VI. Soksi rangi nyeusi
  VII. Raba nyeusi kwa ajili ya michezo rangi nyeupe
  VIII. Truck suti ya kijivu
  IX. **T-SHIT** 2 nyeupe na bukta nyekundu

- **WASICHANA**
  I. Mashati mawili meupe mikono mifupi

II. Sketi mbili ndefu mshono wa **RINDA BOX** mbele na nyuma rangi ya kijani zenye mifukoyakuingia (Utavaa darasani tu)
III. Tai mbili rangi ya sketi (Tai ya kipepeo)
IV. Hijabu ifanane na rangi yas hati
V. Viatu vya ngozi vyenye rangi nyeusi vya kufanga na Gidamu. Visiwe safari boot wala vyenye visigino virefu.
VI. Soksi rangi nyeupe
VII. Raba nyepesi kwaajili ya michezo rangi nyeupe
VIII. Truck suit ya kijivu
IX. T-SHIT 2 nyeupe na bukta mbili nyekundu

**VIFAA VYA DARASANI:**

Mwanafunzi anatakiwa ajena vifaa vifatavyo;

I. Daftari kubwa 20
II. Kaunta book moja la hisabati
III. Mkebe wa mahesabu (Mathetical set) rula na kalamu za wino za kutosha
IV. Penseli na vifutio
V. Kamusiya Kiswahili na dictionary ya kingereza - kiswahili
VI. Awe na begi (School bag) la kebebea vifaa vyake
VII. Rimu bunda moja karatasi nyeupe (A4)

**VIFAA VYA KUJIKIMU KWA MWANAFUNZI WA HOSTELI WANAOKAA MBALI NA SHULE (WASICHANA TU)**

i. Sketi 2 ndefu za kushinda rangi ya damu ya mzee, mshono wa RINDA BOX mbele na nyuma, T-shit mbili nyeusi , kijani (dark blue) itavaliwa baada ya muda wa darasani (t-shit isiwe na maandishi)
ii. Suruali nyeusi yakujikinga na mbu wakati wa masomo ya usiku
iii. Vyombo vya chakula sahani, bakuli ,kikombe na kijiko
iv. Godoro (21/2-6"= nchi sita mashuka mawili ya pinki, mto na foronya zake na blanketi moja.
v. Sanduku la bati (Tranka)
vi. Nguo za kulalia (Night dress)

vii. Rimu ya karatasi nyeupe A4 kwa ajili ya mwanafunzi kujifunzia binafsi.
viii. Vifaa vya usafi binafsi (sabuni, mafuta, malapa, dawa ya meno, mswaki, taulo la pink, ndoo ndogo mbili za plastiki za lita 10 kila moja na ndoo kubwa
ix. Fedha ya matumizi (apewe mwanafunzi) mwenyewe kwaajili ya matumizi yake binafsi
x. Tochi au taa ya betrii pindi umeme unapokuwa umekatika ni muhimu.

**NB:** Nguo za nyumbani haziruhisiwi kabisa hivyo usijenazo shuleni. Muda wauanafunzi wako hapa shuleni unapaswa kuzingatia sheria zote za shule zilizo ambatanishwa hivyo zisome kwa umakini mkubwa.

## MAELEKEZO MUHIMU KWA MZAZI/MLEZI

i. Mzazi mwenye mtoto HOSTEL/BWENINI ataruhusiwa kuja kumtembelea siku ya jumamosi kuanzia saa 2 asubuhi hadi saa 10 jioni
ii. Hataruhusiwa mtu mwingine asiyetambulika shuleni kumtembelea na unapofika usiende bweni na wasiliana na mlinzi mwalimu wa zamu au matroni ili kumuona mwanao
iii. Mwanafunzi hataruhusiwa kwenda nyumbani, hivyo mzazi utatakiwa kumpa mwanao fedha za matumizi na kumletea mahitaji yake muhimu shuleni.

## SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria Na.25 Mwaka 1978. Aidha shule ina zingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu Nchini. Unatakiwa uzingatie mambo yafuatayo ya msingi ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

i. Heshima kwa viongozi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
ii. Mahudhulio mazuri ndani na nje katika shughuli ni muhimu
iii. Kuwepo darasani wakati wa masomo ya jioni (preparation) nilazima
iv. Ni wajibu wakila mwanafunzi kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani au nje ya mipaka hiyo wakati wote wauwanafunzi wako ni lazima
v. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kuzingatia ratiba ya shule kila anapo kuwa shuleni.
vi. Kutunza mazingira na usafi wa mwili wako ni lazima
vii. Ni marufuku kuwa na mavazi au nguo mbali na ulioagizwa
viii. Marufuku kutoka nje ya shule bila ruhusa ya mwalimu wa zamu, matroni au patroni
ix. Maeneo ya fuatayo ni marufuku kwa mwanafunzi kuonekana bila ruhusa ya mwalimu
    a) Makazi ya walimu
    b) Ofisi za walimu
    c) Mabara au chumba cha television (TV room)
    d) Jikoni (Mwanafunzi wa Bweni haruhusiwi kutoka shuleni na siku ya kufunga shule bila mzazi/mlezi kuhusishwa
    e) Mwanafunzi wa Bweni haruhusiwi kutembelewa na mtu mwingine tofauti na mzazi/mlezi wake aliyemleta shuleni na kutembelewa itakuwa siku ya jumamosi saa 2 asubuhi hadi 10 jioni tu, na haruhusiwi kufika Bwenini .Nimarufuku kumletea mwanafunzi chakula kilichopikwa nje ya shule.
    f) Redio na Simu za mkononi ni marufuku shuleni. Vikipatikana vaitavunjwa mbele ya wanafunzi wote.
    g) Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kuingia kwenye Bweni la mwanafunzi wajinsia tofauti.
    h) Mwanafunzi hataruhusiwa kuingia baada ya saa kumi na moja jioni toka nje ya shule.

**MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUFUKUZWA SHULE**

i. Wizi
ii. Uasherati na ushoga
iii. Kuwa na mahusiano ya kimapenzi shuleni (tofauti na uhusiano wa kaka na dada) ubakaji

iv. Ulevi na ,madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi
v. Kupigana au kupiga
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya UMMA
vii. Kudharau bendera yaTaifa
viii. Kuoa au kuolewa
ix. Kupata mimba, kusababisha mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule (kutoamimba)
x. Kugoma, Kuchochea mgomo , Kuongoza au kuvuruga amani na usalama watu shuleni
xi. Kukataa adhabu kwa makusudi
xii. Mwanafunzi kuwa na simu shuleni
xiii. Kushindwa kutunza eneo la usafi kwa kushindwa kupanda maua kutunza mi n.k
xiv. Kuvunja kanuni za shule kwanamna yoyote ile

UNAKARIBISHW SANA KILINDI SEKONDARI

..............................................

JOSEPH CYPRIAN MROKI

MKUU WA SHULE

HEAD MASTER
KILINDI SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 98-SONGE